

COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

THE HANSARD

Thursday, 27th March, 2014

The House met at the County Assembly chambers, Malindi Town, at 2:30 p.m.

[The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala) in the chair]

PRAYERS

MOTION

ESTABLISHING A WHOLESALE MARKET IN THE COUNTY

Hon. Lali: Thank you Madam Speaker. I rise to move the following Motion:-

AWARE THAT small scale business is an important aspect of economic growth in Kilifi County.

AWARE THAT most of our business people depend on Kongowea Market in Mombasa County for various supplies.

AWARE THAT Kongowea Market is expensive to access due to transport costs and congestion.

This honorable Assembly urges the County Executive in charge of Finance and Economic Planning and Land and Physical planning to establish a wholesale market in Mtwapa for ease of access and income generation for the whole of Kilifi County. I now call upon Hon. Kahindi Muhambi to second.

Hon. Muhambi: Thank you Madam Speaker. I stand to second the Motion.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): I now propose the question that this Honorable Assembly adopts the Motion as tabled.

(Hon. Pascal approached the chair and consulted with the Clerk-at-the table and the Temporary Speaker before he moved back to his place)

Hon. Pascal: Thank you Madam Speaker. I have the following amendments to make to this Motion.

Notice is given that the Hon. Pascal T. Jacob intends to move the following amendments to Hon. Lali Omar Sadi's Motion;

That the following words be inserted after the word 'Mtwapa' appearing in the third line of the second paragraph "Mazeras or any other convenient place the County Leadership may find convenient"

The amended motion would read like this:

AMENDED MOTION

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

AWARE THAT small scale business is an important aspect of economic growth in Kilifi County.

AWARE THAT most of our business people depend on Kongowea Market in Mombasa County for various supplies.

AWARE THAT Kongowea Market is expensive to access due to transport costs and congestion.

This honorable Assembly urges the County Executive in charge of Finance and Economic Planning and Land and Physical planning to establish a wholesale market in Mtwapa, Mazeras or any other convenient place the County Leadership may find convenient for ease of access and incoming generation for the whole of Kilifi County.

Thank you Madam Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Anyone to second the Motion?

(Hon Mwachenda stood in his place and nodded)

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Thank you. I now put the question that this Assembly adopts the amendments as tabled.

(Question that amendment be made put and agreed to)

(Applause)

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): I now propose the question that this honourable Assembly adopts the Motion as amended. Any contributions, please? For those honourable members who need to contribute please you are allowed. Hon. Daniel Mangi.

Hon. Mangi: Madam Speaker, I rise to support this Motion. Madam Speaker, I take this opportunity to congratulate Hon. Omar Sadi for bringing this Motion at a really appropriate time.

Madam Speaker, I recall that during the last local authorities' time, I was once the Chairman of Finance in the County Council of Kilifi and at the same time Hon. Lali was the Chairman of the County Council of Kilifi. Madam Speaker, we really saw a lot of bad things happening during the time of local authorities. There was a time when we allocated funds for Mtwapa Market; in fact it was just a matter of availability of land that we did not materialize in that endeavour and adding insult to injury, rampant corruption in the then local authority really made it difficult for the local authorities then to attain such goals.

Madam Speaker, again, revenue collection which is an important denominator and a factor now as regard to this County Government at this early stage of our county is necessary and we need to make sure that we get all the avenues that can enhance revenue collection so that we get the maximum revenue collection in addition to whatever we anticipate from the National Government.

It is therefore important to note that this Motion, if passed into law and implemented, will enable the County Government of Kilifi to get more revenue and at the same time increase income generation to citizens of Kilifi County. It is therefore going to kill two birds with one stone. One; it will increase income for the citizens of Kilifi and number two; we are going to increase revenue in our County Government. It has therefore come at the right time. Honourable Members, let us support this motion and move with speed and pass it so that when it becomes law then the implementors of this law, the Executive, shall again move with speed. They should

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

find land. When we have this market we will be assured that revenue will increase and thus we shall boost our income and infrastructure greatly. Thank you very much, Madam Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Thank you. Hon. Zawadi Christine.

Hon. (Ms.) Christine: Asante Mheshimiwa Spika. Mimi nimesimama kuunga mkono hoja hii nikiwa na haya ya kusema. Tunajua wazi kabisa kuwa wakati huu tuko kwa ugatuzi na ikiwa tuko kwa ugatuzi itakuwa ni aibu Kaunti ya Kilifi nzima tuwe tunategemea Kaunti ya Mombasa kwa ajili ya kuletea watu wetu vyakula ama bidhaa.

Kwa hivyo, ni wakati mwafaka mjadala huu umekuja ili uwe ugatuzi kamili ili nasi pia tupate soko. Watu wetu mara nyingi vitu vyao vinaozea njiani wakienda kwa soko kwa sababu kufika sokoni na mapema inakuwa shida na hata wakifika huwa kuna milolongo ya magari kuanza Kongowea mpaka pengine darajani huko. Inakuwa vitu vinaozea hapo wakiwa wanangojea nafasi na wao waingie ndani ya soko.

Sasa basi ikiwa hili soko litajengwa ndani ya Kaunti yetu tutaingiza pesa na mbali na kuingiza pesa itakuwa tumerahisishia pia watu wetu kufika sokoni wakati ufao na kuuza mauzo yao kwa wakati ufao. Nimesimama kuunga mkono hoja hii.

The Temporarily Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Asante Mheshimiwa Christine. Mheshimiwa Nashee.

Hon. (Ms.) Nashee: Asante Mama Spika. Mimi naunga mkono hoja hii na hata kumshukuru Mheshimiwa Lali kwa kuitanguliza lakini mimi pia naona ningeileta kwa sababu mimi nina mambo fulani ambayo yangenifanya nilete hoja hii ili tutetee hii Kaunti ya Kilifi ili nasi tuwe na soko kubwa kama la Kongowea ili tupate kujenga Kaunti yetu.

Kwa sababu hiyo yale magari ambayo yanatoa chakula kutoka Nairobi yakileta Kongowea yanapitia pale Mariakani kwetu na Mariakani iko katika Kaunti ya Kilifi, yanapitia pale Mazera kwetu na Mazera iko katika Kaunti ya Kilifi na watu wa Kilifi wanapata shida kwenda Mombasa. Sisi tuko na njia yetu ya Kaloleni kufika Mombasa ambayo ni rahisi. Wanaweza kuchukulia vitu Kilifi ikiwa watachukulia Mazera; kwetu kuna barabara ya nyuma inatokezea Kilifi mpaka Malindi. Sasa sisi wenyewe tutajifaidika kwa pesa zetu na watu wetu watakuwa wamerahisishiwa kibiashara, na itakapokuwa sisi tumepanga mambo yetu ya kilimo pia tutakuwa tumeipanua Kaunti yetu ya Kilifi. Mimi naunga mkono hoja hii lakini naomba lile soko liwe Mazera ama Kaya Fungo. Asante Madam Spika.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Yes Mheshimiwa Mlanda.

Hon. Mlanda: Thank you Madam Speaker for giving me this opportunity to express my views regarding this Motion.

I take this opportunity to congratulate Hon. Lali and Hon. Pascal for the amendments. Madam Speaker, we have been traveling to Mombasa sending our commodities there which is very expensive for the common mwananchi to go and buy some commodities at Kongowea.

Madam Speaker, this Motion has really come at the right time that we are trying to make Kilifi County a better place to stay in. It will be very ideal to have this market built in our County so as to reduce the cost of travelling and the cost of the commodities whereby our people will easily access commodities within our county. In addition to that, Madam Speaker, it will create job opportunities for youth and women.

Madam Speaker, I stand to support this Motion and urge the committee in charge to move faster so that we can also reap the revenue from the business community. Thank you very much, Madam Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Thank you Hon. Mlanda. Hon. Mwachenda.

Disclaimer: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor

Hon. Mwachenda: Asante sana Mheshimiwa Spika. Mimi pia nasimama kuunga mkono hoja hii kwa sababu mbili; ya kwanza ni kwamba Kaunti ya Kilifi ni moja ya zile Kaunti huru katika taifa la Kenya na kusema kweli tulivyo huru yatakikana pia tuwe na vitu vya kujitegemea wenyewe mojawapo ikiwa ni soko.

Itakuwa jambo la kusikitisha kwamba sisi tukitaka kufanya biashara lazima tuingie katika Kaunti ya Mombasa ili tuweze kunufaisha biashara zetu. Lile ni jambo la kusikitisha na la aibu. Kama ni ardhi tuko nayo; kama ni uwezo tuko nao. Ni afadhali tuweze kupitisha ili sisi tuweze kuwa na soko letu kubwa kama lile.

Sababu yangu ya pili; leo tumejiwekea twataka tuwe na Bilioni mbili kama ushuru ambao tutakuwa tukikusanya kama Kilifi Kaunti. Ikiwa hatutakuja na vitu vya kuweza kutengeneza ushuru kama ule basi lengo letu la kukusanya ule ushuru wa Bilioni mbili hatutaweza kulifikia. Kwa hivyo, moja kwa moja mimi naunga mkono swala hili na ikiwa itaweza kupita niko na imani kubwa kwamba si ajabu hata nusu ya yale malengo yetu ya ule ushuru tutaweza kuyatimiza. Asante.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Thank you Hon. Mwachenda. Hon. Barka.

Hon. (Ms.) Barka: Asante Bi. Spika. Nampongeza Mheshimiwa ambaye ameleta hoja hii na haswa yule aliyeifanyia marekebisho.

Hii ni kwa sababu ukiangalia Kaunti ya Kilifi hii bado tuko na ardhi tena nyingi sana na tunajivunia na haswa wakati wa manispa ardhi nyingi wananchi walizichagua ziwe sehemu za soko lakini hatujui ndio ulafi wa mabwenyenye ama waliokuwa hapo bado wamezikalia. Ardhi hizo zingekuwa zinawasaidia wananchi wetu waliotoa hoja kwamba wajengewe soko.

Tukiangalia vizuri kama upande wa Mijomboni kuna ardhi nzuri pale na ilipimwa vizuri lakini tunashangaa mpaka dakika hii tunangojea kitu gani kwani soko hilo bado halijajengwa. Dadangu ameongea vizuri kwamba ugatuzi inamaanisha watu wapate huduma karibu. Ikiwa mpaka sasa masoko hayo hayajajengwa tunatarajia wananchi wale washerehekee ugatuzi vipi? Tukiangalia sisi ambao ni wanakamati wa Planning, Mipangilio na pia upande wa Kilimo, kwenye mipangilio kumbukumbu ile tulisema kilimo lazima tukipatie kipaombe. Ikiwa sisi wenyewe tunajipangia vitu vyetu tuvipeleke Kongowea, kweli jamani ni haki? Wenzangu waheshimiwa naomba ikiwa itawezekana sote kwa pamoja tuweze kuunga mkono kila mahali ambapo pana ardhi, mwananchi ni lazima asaidike apate mazao ya kutoka Kaunti ya Kilifi karibu na shilingi zetu mbili tatu za Kaunti ya Kilifi zitufaidishe sisi wenyewe. Asante.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Thank you Hon. Barka. Hon. Muthoka.

Hon. (Ms.) Muthoka: Asante sana Madam Spika. Mimi nami nasimama kuunga mkono hoja hii na namshukuru Mheshimiwa Lali kwa kuleta hoja hii. Kama wenzangu walivyotangulia kusema, Kaunti ya Kilifi tunatakikana tuwe na soko; ardhi tunayo ya kutosha. Itakapofika wakati wa lile soko hatusemi tu soko kama Kongowea, ningesema tunataka tuwe na soko ambalo limepangwa kwa mpangilio mzuri; maana soko la Kongowea ni soko kweli lakini hilo soko ni chafu sana. Inatakikana soko la Kilifi Kaunti lipangiwe ili liwe ni soko ambalo wana Kilifi tunaweza kujivunia maana ardhi ya kutosha tunayo.

Haina haja ya tuvute; tusipeleke soko mahali kuna ardhi ya kutosha bali tuweke soko zuri mahali ambapo hata sisi wana-Kilifi tunakuza vitu mahali hapo. Kuna maembe yanatoka hapa na tunaona watu wanatoka Mombasa na sehemu nyingine mbali mbali kuja kukusanya na kupeleka Kongowea. Tunataka hayo maembe tuuze katika soko la Kaunti ya Kilifi maana yanatoka katika Kaunti ya Kilifi ili tuzidi kuinua uchumi wa Kaunti hii.

Vile vile kuna vitu vingine kama mboga ambazo zinatoka Chakama na pia kuna nazi zinazotoka hapa zikipelekwa Taveta. Tunataka vile vitu ambavyo vinatoka Kaunti ya Kilifi kuwe

Disclaimer: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor

na soko ambalo litawezesha vitu kutoka Taveta bali si mteja akutane navyo njiani na aje Kaunti ya Kilifi. Uchumi wetu wa Kilifi Kaunti uinuke kupitia kwa mimea tunayoikuza mahali hapa na soko mwafaka lijengwe soko. Soko liwe na nafasi maridadi ambayo hata kukinyesha mvua halitatutaliza na kisha kuwe na mahali pa kugesha magari pa kutosha. Asante sana.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Thank you Hon. Muthoka. Hon. Mwingo.

Hon. Mwingo: Asante sana Mheshimiwa Spika kwa hii nafasi. Mimi pia vile vile nachukua hii nafasi kuunga mkono msawaada huu ambao umeletwa kwa sababu moja. Sababu yangu ni kwamba ndani ya Kaunti ya Kilifi wengi sana tumetegemea kilimo na mpaka hivi tunavyoongea kuna wakulima wengi sana ambao hawajui zile mali zao wataziuza wapi. Vile vile kuna mavuno mengi ambayo yako hapa ndani ya Kaunti ya Kilifi lakini hata yule mkaazi wa kule Mtwapa bado hajajua kwamba mavuno yale yanaliwa na wanadamu.

Kwa hivyo itakuwa vizuri tukiwa na soko letu hapa Kilifi ili yule wa kule mbali ambaye analima mananasi, kuna wengine wana miti ya *Mubono*, na ambapo *Mubono* huwa unatengenezwa mafuta mazuri sana. Yule mama anaweza kuvuna *Mibono* awe na mahali ambapo anaweza kuiuza.

Ndani ya Kaunti ya Kilifi kuna vyakula vingi ambavyo watu bado hawajajua umuhimu wake. Tukiwa na soko letu hapa tutakuwa na nafasi ya kuuza kama ni *Mzungi*, kama ni kila aina ya mboga ambazo wengine kule bado hawajajua ya kuwa zina umuhimu sana hata katika sherehe zetu. Kwa hivyo, mimi ninaunga mkono ya kwamba tuwe na soko letu katika Kaunti ya Kilifi ambalo litatusaidia. Asante Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Thank you Hon. Mwingo. Hon. Pascal.

Hon. Pascal: Asante sana Mheshimiwa Spika. Mimi vile vile ninaunga mkono hoja hii kwa sababu tunaona ya kwamba wakulima wamekuwa wakiteseka sana kule Kongowea kwa sababu hakuna soko lingine mbadala ambalo litaleta mashindano ya kikamilifu kibiashara.

Tunaona watu wanaenda pale asubuhi kupeleka bidhaa zao na wakifika pale bei za vitu zimebadilishwa bila kuarifiwa. Kwa hivyo inakuwa ni msongamano wa hapa na pale na hii imesababisha mazao kuharibika njiani na mazao mengine kuozea pale kwa soko bila kuingia sokoni na hali kadhalika. Kwa hivyo ninaunga mkono tupate soko letu kama watu wa Kilifi.

Juzi tulikuwa na Mheshimiwa Rais, alikuja pale kuanzisha huu mradi wa kunyunyuzia mimea maji na hiyo ina maana ya kwamba baada ya muda si mrefu tutakuwa na bidhaa nyingine ambazo zitahitaji kuuzwa. Kwa hivyo, tukiwa na soko letu litatusaidia sana kuuza zile bidhaa ili tuone ya kwamba na sisi tunaongeza na tunainua uchumi wetu wa Kilifi.

Vile vile kama wenzangu walivyosema itakuwa ni njia moja ya kutoa ajira kwa watu wetu ambao wamemaliza kusoma lakini hakuna mahali wanakoenda. Kwa hivyo, itakuwa ni njia bora ya kuona ya kwamba hali ile ya ukosefu wa kazi tunaweza kuisaidia. Ninasimama kuunga mkono kabisa hoja hii. Asante sana.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Thank you Hon. Pascal. Hon. Jared Kaunda.

Hon. Kaunda: Mimi nasimama kuunga mkono hoja hii ambayo imeletwa na ndugu yangu Mheshimiwa Lali. Madam Spika, Mswada huu umekuja kwa wakati ambao unafaa. Mimi naweza kutoa ushahidi wa kuona kwamba Kilifi tuko na umuhimu wa kupata hili soko; ikiwa mimi ni mkulima wa mananasi hivyo ninavyokuambia, Madam Spika, jana nilitoa mzigo wangu shambani nikapeleka Kongowea. Soko limejaa hata sikuweza kupakua mpaka leo ndio wameweza kupakua mzigo.

Madam Spika, mali ile iko na thamani ya zaidi ya laki moja unusu na saa hii ikiteremshwa kwa sababu tunavyojua matuda ni vitu ambavyo ni hafifu vinataka vikichukuliwa vifike kwa soko wakati unaostahili. Saa hii ninavyokuambia Madam Spika niko na mali ambayo

Disclaimer: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor

itatupwa ambayo inafikia robo ya ile mali ambayo kama kungekuwa kuna soko hapa mali ile ingeweza kufika bila msongomano.

Vile vile naweza kutoa ushahidi kwamba gari lile ambalo nilikomboa kutoka shambani mpaka Mombasa nilikomboa kwa Shilingi 45,000.

Madam Spika itakuwa muhimu kuona kwamba tukiwa na soko hapa itatuwezesha sisi kupata angalau afueni hata kwa usafiri, itakuwa huwezi kuchukua lori hapa na ulipe Shilingi 45,000 hapa mpaka Mombasa, halafu mali ikaharibike.

Mimi nasimama kuunga mkono mswada huu na ninaona kwamba umekuja kwa wakati unaofaa. Waheshimiwa wenzangu, tuweze kuunga mkono hata kama pesa zetu zitakuwa hazitoshi lakini hata kama tutaangazia pale pamoja angalau katika Kaunti ya Kilifi tuweze kupata soko ambalo linaweza kusaidia wakulima basi itakuwa bora sana. Asante sana Madam Spika. Nasimama kuunga mkono Mswada huu.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Thank you very much. Hon. Wanje Chiku.

Hon. (Ms.) Chiku: Thank you Madam Speaker. I stand to support the Motion. Madam Speaker, a Market is the backbone of any County and a market generates a lot of revenue if properly designed.

It is a shame to say that there is an open-air market and the county is collecting a lot of revenue while the people in that market sit under the sun the whole day and sometimes they are rained on. Let us have a modern market Madam Speaker which will serve our people well. Thank you.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Hon Fondo.

Hon. Fondo: Mheshimiwa Spika mimi nami naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Lali kwa sababu hizi ambazo zinafwatia. Tunajua Mheshimiwa Spika ya kwamba kilimo biashara ndio sasa katika Kaunti ya Kilifi tunaangazia zaidi.

Tukiangalia kwa mfano juzi Mheshimiwa Rais Uhuru Kenyatta alizindua mradi wa unyunyuziaji maji kule Kulalu Ranch, Galana, ekari Milioni moja. Ekari 1,000,000 ambazo hizo saa hii shughuli zimeanza na itakuwa ni aibu Mheshimiwa Spika ya kwamba tutakuwa tunatengemea soko la Kongowea peke yake; mazao yale yale kutoka Kulalu ama Galana Ranch yaweze kutolewa kule yapite ndani ya eneo bunge la Magarini yaingie Malindi kuelekea Kongowea.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika mimi naunga mkono moja kwa moja mswada huu ili tuweze kupata soko katika Kaunti hii yetu ya Kilifi.

Vile vile Mheshimiwa Spika juzi nilitembelea sehemu mbili na Mheshimiwa Waziri; tulikuwa kule Gandini ambako wanafanyia uuzaji maji, kulima mchicha, mnavu, ndizi, paipai na mananasi vile vile. Basi Mheshimiwa Spika niliona ndizi na paipai ambazo hata ukienda soko la Kongowea hutaweza kuziona. Mapaipai ambayo paipai moja ni zaidi ya kilo ishirini; basi wanashindikana kwamba wabebe mapaipai yale kuelekea kutafuta soko kule Mombasa ambapo wanaweza kupata bei nzuri. Hii ni kwa sababu sisi katika Kaunti ya Kilifi hatuna soko ambalo mazao yale yanaweza kuuzwa katika sehemu hii ya Kaunti yetu.

Mheshimiwa Spika lingine ni kwamba, ni aibu Mheshimiwa Spika wewe unaweza kutoka hapa ukienda ile steji ya Malindi unakuta magari yametoka Chakama kuleta mnavu, mchungu pale na ile ni steji lakini hasa unaona Mheshimiwa Spika hawa kinamama wanaweka rejareja hata wewe ukiwa unatamani hiyo mboga huwezi kuenda kununua kwa sababu inawekwa kwa barabara; nyanya na pilipili zinawekwa pale hata mimi au hata wewe Mheshimiwa Spika huwezi kujisikia kununua mboga zile.

***Disclaimer:** The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Hii ni aibu katika Kaunti hii; tunahitajika tupate Soko letu ili tuweze kusaidia hawa wakulima ambao ni wakulima biashara waweze kupeleka mazao yao. Mheshimiwa Spika, niko hapa kuunga mkono hoja hii. Asante sana.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Hon. Arafa.

Hon. (Ms.) Arafa: Thank you Madam Speaker. I stand to support the Motion, and I congratulate the Hon. Member who brought this Motion to this House and the one who did the amendment.

A market is key to improving our economy in the County of Kilifi. I will urge that we first do a feasibility study for this market; we can construct on land which is not accessible. Before we construct that market, we have to improve our infrastructure; roads, electricity and come up with storage facilities for these products from our farms. It is high time that as we identify this land, we also make sure that infrastructure is first in place.

One other thing is that we have to come up with a modern system of marketing our products. We should have different classification; we are not constructing for farm products only but we should also focus on fisheries. We have a lot of fish and Marine products which it is not only fish but also crabs and other products.

Another thing we can also do is use the market as a tourist attraction center. Most of the tourists come down here and we see them walking around in our market but at the end of the day they see the negative side of us for not having well constructed and good hygienic markets. We want them to come and see the best of us; how we run market facilities in our county. I urge the Honourable members in this House that in the 2014/2015 budget, let us set aside huge amounts of money to come up with this market and I am very sure in the next five years Kilifi County won't be recognized as one of the poorest counties anymore; the county will improve its economy from 47 to maybe 40 or 30 in the 47 Counties in Kenya. Thank you very much.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Yes Hon. Matsaki.

Hon. Matsaki: Asante sana Madam Spika. Mimi pia nimesimama kuunga mkono hoja ambayo iko mbele yetu. Hoja hii imeletwa wakati mzuri. Baada ya yale yote ambayo yamezungumzwa na waheshimiwa ni dhahiri kwamba Kaunti ya Kilifi haina soko na ikiwa watu wametoka mbali zaidi mpaka waende wafike Kongowea inaonekana pia ile gharama ya kufikisha bidhaa zetu katika soko la Kongowea iko juu.

Kwa hivyo mimi naunga mkono angalau tupate mahali ambapo tunaweza tukawa na soko letu ili watu wa Kaunti hii waweze kupeleka bidhaa zao pale.

Vile vile nataka niseme kwamba hata Mheshimiwa ambaye pia amejaribu kuweka mabadiliko kidogo utakuta kwamba kutoka Mariakani, Kaloleni na Magarini kote wanazunguka upande ule. Ingekuwa ni vizuri kama upande ule mwingine kutapatikana mahali tuweze kupata hilo soko. Kwa hivyo, nimesimama kuunga mkono hoja hiyo. Asanteni sana.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Thank you Honourable members. I will now allow the mover to the Motion to make his final submission.

Hon. Lali: Asante sana Madam Spika. Nataka kuchukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wenzangu wote kwa kuchangia mswada huu. Tumekuwa na kikao tukalizungumzia swala hili mpaka tukaona ni muhimu kuwe na majadiliano katika bunge hili, na pia nataka kumshukuru kwa dhati mweshimiwa Mchungaji Pascal kwa kuleta mabadiliko katika hoja hii.

(Applause)

Hon. Lali: Waheshimiwa wenzangu nataka kuwaambia kwamba Mheshimiwa Gavana wetu wa jimbo hili miongoni mwa ahadi zake wakati wa kampeni ilikuwa ni kuweka miundo msingi dhabiti ya kuinua uchumi wa jimbo hili.

Mkiangalia miongoni mwa watu wetu wengi wametegemea kilimo kama njia ya kupatia maishani, aidha ikiwa ni kilimo chakula ama mfugo ama ni uvuvi. Soko kama hili litasaidia watu wengi kwa kipande kikubwa kufanya biashara ama kujiingiza katika biashara.

Pili ningependa muliangalie jimbo la Kilifi pale lilipo, jimbo la Kilifi limeshikana na Mombasa, limeshikana na Kwale, limeshikana na Taita Taveta, limeshikana na Tana River ambayo pia ni Lamu. Ikiwa Mombasa wana soko na hawalimi kitu biashara yote tunachukuwa na tunawapelekea wao, ni wakati mzuri ya kwamba sisi tuangalie pahali mwafaka ambapo tunaweza kufanya biashara tukainua uchumi wa kwetu.

Pahali palipo pendekezwa kama Mazeras, ukiangalia Mazeras ile barabara inakusudiwa ya by-pass yatoka na Mazeras-Mombasa imeshikana na Mazeras, watu wa Pwani wanategemea chakula kingi sana kutoka nyanja za juu na magari yote ya njanja za juu yanapitia Mazeras ndio yaiingie Mombasa. Waheshimiwa wenzangu nataka kuwaambia kwamba soko hili likijengwa litainua uchumi wetu na kutupa kipato sisi kama jimbo.

Vilivile nataka kuongezea kuwa hili soko kujengwa ni sharti tujenge soko la kileo. Hata kama kutatoka kamati husika iweze kuangalia ni nchi gani imetengeza soko la kileo, kukitengenezwa soko kuwe na soko litakalo weza kubeba chakula cha kilimo, nyama ya mifugo mbalimbali, samaki wa kutoka kwa wavuvi mbalimbali viwe vinachukuliwa katika soko hili. Na sheria ya kiserikali imetupa ruhusa ya kwamba tunaweza kujenga soko hili aidha kwa mfuko wetu wenyewe ama kushirikiana na wafadhili wa sehemu mbalimbali. Kwa hayo machache nataka kuwaambia waheshimiwa shukrani na Mwenyezi Mungu awabariki. Asante sana Mheshimiwa Spika.

(Applause)

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Asante Hon.Lali. I will now go through the question that this Assembly adopts the Motion as amended.

(Question put and agreed to)

(Applause)

ADJOURNMENT

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): There being no any other business, this House stands adjourned till Tuesday 1st April, 2014 at 2.30 p.m. Thank you.

The House rose at 3:10 p.m.

Disclaimer: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor

***Disclaimer:** The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*